


## Mtazamo wa kimkakati wa NCIC

Mtazamo wa kimkakati wa NCIC umejishikilia katika sehemu tano kuu zifuatazo:

1. Kuunda na kuwezesha asasi mbali mbali pamoja na Umma katika kuleta thamani na umoja wa kitaifa.
2. Kutangaza amani ya kitaifa, maridhiano, uwiano na utangamano kati ya makabila, mbari na makundi ya kidini ya Kenya kupitia njia za kuunda mahusiano mema maridhiano.
3. Kuhakikisha ufuatiliaji wa Sheria na kanuni bora zitakazoimarisha uwiano na utangamano.
4. Kufanya utafiti na mafunzo katika masuala yote yanayohusiana na ukabila na kutoa mapendekezo kwa Serikali.
5. Kuwezesha NCIC ili waweze kutekeleza majukumu yao kikamilifu na inavyohitajika kuambatana na Katiba ya Kenya, 2010.

## Mfanikio

NCIC imetoa mchango mkubwa katika kujenga jamii ya Wakenya iliyo na uwiano na utangamano. Hii ni pamoja na:

- Mbinu za kutatua migogoro ya kikabila na kidini, pamoja na kuzuia vurugu na kufanya mabadiliko.
- Matumizi ya kifungu cha Sheria ya NCI, na hususan katika Kauli ya Uchochezi. NCIC huchunguza madai na malalamishi yanayotolewa kuhusu dhulma, usumbufu na kauli za uchochezi kwa lengo la kuleta Uwiano na Utangamano wa Kitaifa kama ilivyo katika sheria ya NCI ya 2008.
- Tume hii imepigania kushirikishwa kwa Uwiano wa Kitaifa shuleni hasa kwenye mitalaa na sera za elimu pamoja na kuunga mkono michezo shuleni, kama vile Drama na matamasha ya muziki.
- Tume imekuwa ikisaidia uundwaji wa Vilabu vya Amani katika asasi mbali mbvali za masomo, licha ya kuwepo kwa ushirikiano mwema na Maafisa Wasimamizi wa Kielimu wanaoshughulikia masuala ya uwiano na utangamano.
- Kuhimiza ushirikishwaji wa matumizi ya pamoja ya rasilimali za Kitaifa na zile za Serikali za Kaunti kupitia kwa Ukaguzi wa Kikabila.
- Kuwepo kwa mijadala wazi kuhusu masuala ya ukabila na kuukubali uanuai wa kikabila kupitia kwa mazungumzo.
- Walichangia katika kusababisha kuwepo kwa amani kwenye Kura ya Maoni iliyofanyika 2010 pamoja na Uchaguzi Mkuu wa 2013.
- Kuwawezesha wanahabari na kuwapa maelezo ya kutosha wahusika wa vyombo vya habari katika njia za kulete amani na kutatua migogoro.
- Kuwawezesha viongozi wa Wanawake na Vijana kushiriki vilivyo katika njia za kuimarisha amani na kutatua migogoro.
- Kufanya utafiti na kuchapisha masuala yanayohusiana na uwiano.
- Kuingiza kanuni za Uwiano na Utangamano katika Miswada:
- Kushirikisha Kanuni za Uwiano na Utangamano wa Kitaifa katika huduma za Umma.
- Kushirikiana na asasi nyingine za Umma, mashirika ya kijamii, vyombo vya habari na washirika wa kimaendeleo, kati ya wengine wengi.



*Tume ya Kitaifa ya Uwiano na Utangamano*
*KMA Centre 6th Floor, Mara Rd, Upper hill*
*S.L.P. 7055-00100*
*Nairobi, Kenya*
*+254 -20-2585702/3/1. Ext. 131.*
*http//:www.cohesion.or.ke*
*twitter.com/NCIC Kenyapage*
*facebook.com/NCIC Kenya (Cohesion)page*

NATIONAL COHESION AND INTEGRATION COMMISSION
PAMOJA

## *Watu Wamoja, Taifa Moja, Hatma Yetu*





## Kuhusu Tume ya NCIC

Tume ya Kitaifa ya Uwiano na Utangamano (NCIC) ni shirika lililoanzishwa kisheria chini ya kifungu cha sheria nambari 12 ya 2008 inayohusu Uwiano na Utangamano wa Kitaifa. Kuanzishwa kwa Tume hii kuliitambua haja ya kuwepo kwa taasisi ya kitaifa itakayojenga uhalisia na thamani ya kitaifa, kupunguza mashindano ya kisiasa na kijamii pamoja na vurugu za kisiasa, kupunguza dhulma za kikabila, mbari na kidini na pia kutangaza maridhiano na umoja wa kitaifa.

## Maazimio

Kuwa na jamii ya wakenya yenye Amani, Uwiano, Ushirikiano na Utangamano.

## Malengo

Hakikisha kuangamizwa kwa aina zote za dhulma za kikabila na kutangaza uwepo wa huruma, maelewano thabiti, pamoja na kukubali uanuai, ili kuishi kwa ushirikiano na umoja.

## Thamani Maalum

- Utaalamu
- Maadili mema
- Maamuzi maalum kuhusu makundi ya watu waliotengwa na walio wachache
- Uhusishwaji pamoja na Kuheshimu Uanuai

## Majukumu Yetu

Kuandaa na kutangaza nafasi za kazi, mtagusano na mahusiano mema kati ya watu wa makabila mbali mbali, dini pamoja na mbari za jamii tofauti tofauti za Kenya, na hali kadhalika kuishauri serikali kuhusu masuala mbali mbali.

## Malengo ya Tume

1. Kuandaa na kutangaza nafasi za kazi, mtagusano na mahusiano mema kati ya watu wa makabila mbali mbali, dini pamoja na mbari za jamii tofauti tofauti za Kenya, na hali kadhalika kuishauri serikali kuhusu masuala mbali mbali.
2. Kuangamiza njia zote mbovu za dhulma za kikabila na kimbari pamoja na kuhimiza watu, asasi, vyama vya kisiasa na mashirika mbali mbali kutotangaza ama kupigia debe dhulma.
3. Kuhimiza kuwepo kwa masikilizano, maelewano na ukubalifu wa uanuai katika nyanja zote za maisha ya kitaifa.
4. Kutangaza na kuheshimu tamaduni za kidini pamoja na uanuai wa lugha katika jamii ya kila mkenya.
5. Kupanga, kusimamia, kuendesha na kutangaza miradi ya elimu na mafunzo ili kuufahamisha umma, kuunga mkono na pia kuimarisha amani na umoja kati ya jamii za makabila yote na koo za makundi mbali mbali;
6. Kutangaza maafikiano, maridhiano, majadiliano na njia nyinginezo kama hizo ili kutafuta mifumo bora ya suluhu dhidi ya migogoro na vurumai.
7. Kuchunguza malalamishi kuhusu dhulma na kufanya mapendekezo kwa Mwanasheria Mkuu, Tume ya Haki ya Kibinadamu ama halmashauri nyinginezo katika njia za kutafuta suluhu itakayochukuliwa kwenye sehemu ambayo malalamishi hayo yatafaa.
8. Kuchunguza utendakazi wake ama kupitia ombi kutoka kwa taasisi yoyote, ofisi, ama mtu kuhusu suala lolote linaloathiri uhusiano wa kikabila na kimbari.
9. Kuanzisha, kupigia debe na kushughulikia mabadiliko ya sera, sheria pamoja na usimamizi katika masuala yanayoathiri mahusiano ya kikabila.






10. Kufanya utafiti na mafunzo pamoja na kuandaa mapendekezo kwa Serikali kuhusu masuala yoyote yanayohusiana na hali ya ukabila ikiwa ni pamoja na kupima iwapo uhusiano wa kikabila unaimarika.
11. Kuchunguza na kutoa ripoti kwa Bunge la Kitaifa kuhusu hali halisi na mafanikio ya kutekeleza mapendekezo hayo.
12. Kufanya maamuzi ya kimkakati na kutoa kipaumbele katika sera za kimaendeleo ya kiuchumi-jamii, kisiasa ambazo zinaathiri pakubwa mahusiano ya kikabila na hatimaye kutoa ushauri wa jinsi ya utekelezwaji wake.

## Mfumo wa Kiusimamizi

Tume hii ina Makamishna pamoja na afisi ya usimamizi. Makamishana wa Tume ni pamoja na Mwenyekiti akiwa na makamishna saba (7) walioteuliwa na Rais baada ya kuidhinishwa na Bunge la Kitaifa.

Mwenyekiti wa Tume ya Kitaifa ya Haki za Kibinadamu, Mwenyekiti wa Tume ya Kitaifa ya Usawa na Jinsia pamoja na Mwenyekiti wa Tume ya Usimamizi wa Haki (Afisi ya Mjumbe wa Wananchi).

Afisi ya Usimamizi inasimamiwa na Katibu wa Tume/Mkurugenzi Mtendaji, na wafanyikazi wengine wanaohudumia kwenye idara mbili kuu ikiwa ni pamoja na Idara ya Usimamizi na Fedha; na Mipango na Huduma za Kitaalamu.

